## Mavunde anena na ma-CEO>

**Dodoma.** Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira Antony Mavunde ameitaka bodi ya wakurugenzi wa CEO Roundtable kuwasilisha Serikalini changamoto na mapendekezo yatakayosaidia ukuaji wa sekta binafsi.

Akizungumza katika kikao na wajumbe wa bodi hiyo, Mavunde alisema kuwa Tanzania ina watu wenye nguvu kazi ya kufanya kazi milioni 22.3 lakini changamoto kubwa inayowakabili ni ujuzi walionao. (**Sharon Sauwa**)



## Samia akumbuka walemavu

**Shinyanga.** Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan ameiagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha mitaala inapobadilishwa inaendana na ubadilishaji vifaa vya kufundishia ikiwemo ya wenye mahitaji maalum ili kuondoa usumbufu. Akizungumza na watumishi na watoto wenye ulemavu jumuishi katika kituo ch Buhangija, Shinyanga alisema Serikali itahakikisha inasomesha walimu wa elimu maalumu ili kutoa fursa kwa kundi hilo. (**Stella Ibengwe**).

## Kwa Ufupi

### Raia wa Kenya jela miaka 12

**Moshi.** Raia wa Kenya, Josephine Mumbi Waithera amehukumiwa kifungo cha miaka 12 jela na kulipa faini ya Sh480 milioni baada ya kupatikana na hatia ya kusafirisha dawa za kulevya.

Raia huyo wa Kenya alikamatwa Juni 4, 2012 katika Uwanja wa Ndege wa Kia akisafirisha kilo 3,249 za heroin kwenda Vienna nchini Austria.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Moshi, Pantricia Fikirini.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, wakili wa

# RC amaliza mgomo wa wauza nyam

Sada Amir, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Mwanza.** Mgomo wa wafanyabiashara na wachinjaji wa ng'ombe jijini Mwanza uliosababisha wakazi wa jiji hilo kukosa nyama kwa siku mbili mfululizo kuanzia Februari 25 sasa umemalizika.

Mgomo huo umemalizika baada ya mkuu wa mkoa huo, John Mongella kuingilia kati mgogoro kati ya wafanyabiashara, wachinjaji na uongozi wa halmashauri ya jiji hilo uliotokana na ushuru unaodaiwa kusababisha gharama kubwa ya biashara.

Akizungumza na wafanyabiashara hao alipotembelea mnada wa Nyamatala wilayani Misungwi juzi, Mongella aliagiza wafanyabiashara kuendelea kutoa huduma wakati malalamiko yao yakitafutiwa ufumbuzi ndani ya siku saba kuanzia Februari 26.

Kwa mujibu wa mwenyekiti wa umoja wa wafanyabiashara soko kuu jijini Mwanza, Hamad Nchola, wafanyabiashara na wachinjaji waligoma kupinga ushuru na tozo unaofikia Sh33,300 kwa kila ng'ombe kuanzia mnadani, usafirishaji, uchinjaji na usafirishaji wa nyama.

Mgomo wa wafanyabiashara na wachinjaji ulileta neema kwa wafanyabiashara wa samaki na kuku baada ya wakazi wa jiji la Mwanza kugeukia vitoweo hivyo na hivyo kufanya bei kupanda.



"Endeleen kutoa hud ma wakati malalamik yenu yakitafutiwa ufumbuzi ndani ya siku saba."

Mongella

## AFYA

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan akiuliza maswali kwa uongozi wa Chuo Cha Ualimu Shycom,

